# GRADE 5

# KISWAHILI

# END-TERM-2-2023

| Kuzidisha matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
|---|---|---|---|
| 4<br>20 - 30 | 3<br>11 - 19 | 2<br>6 - 10 | 1<br>0 - 5 |

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 5.**

Rosa alikuwa kigoli wa miaka sita. Alizaliwa na wazazi wake wachochole kupindukia. Mama yake hakuweza kusoma kwa sababu ya ukosefu wa karo. Walikuwa **wakilalia mate** mara kwa mara. Mama yao alipoona mzigo wa kuwalea ulimlemea aliondoka nyumbani asijulikane alikoenda. Naye Rosa aliteseka sana na ikambidi naye aondoke nyumbani asijue alikoenda mradi awe mbali na nyumbani kwao kulikojaa shida.

Licha ya umri wake mdogo, Rosa aliajiriwa katika shamba la mibuni. Hata kulala alilala huko. Huko alikutana nawatoto wengine waliotumia dawa za kulevya ili kujaribu kusau shida walizokuwa wakipitia.

1. Wazazi wake Rosa walikuwa
   A. maskini B. matajiri
   C. walemavu D. wasomi
2. Maneno '**wakilalia mate**' yamepigiwa mstari katika kifungu. yana maana gani?
   A. wakilalia juu ya mate
   B. walikula mate
   C. waliongea usiku mzima
   D. walilala njaa
3. Mama yake Rosa aliondoka nyumbani kwasababu ya
   A. njaa
   B. mateso
   C. ukosefu wa karo
   D. kumtafuta mwanawe
4. Licha ya umri wake, Rosa
   A. aliajiriwa mkahawani
   B. alienda shuleni
   C. aliajiriwa katika shamba la mbuni
   D. aliajiriwa katika shamba pareto
5. Kwa nini watoto walitumia mihadarati?
   A. Kujistarehesha
   B. Kujisaulisha shida zao
   C. Hawakuwa na kazi
   D. Walikosa adabu

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 6 hadi 9.**

usafi ni jambo muhimu ambalo linapaswa kushughulikiwa na watoto na watu wazima. Kuna usafi wa mwili na wa mazingira. Katika usafi wa mwili kunayo mengi ya kuzingatia. Kucha zetu ni lazima zikatwe ili uchafu usipate mahali pa kujificha. Nywele nazo zioshwe na ziwe fupi ili vimelea

wanaoitwa chawa wasipate makao. Meno yetu yanapaswa kupigwa ili kuondoa ugavu ambao unaweza kufanya kinywa kinuke na kuoza kwa meno. Pua zetu nazo ziwe safi daima. Tupenge kamasi kwa hanchifu safi kuondoa kamasi.

6. Usafi unapaswa kuzingatiwa na nani?
   A. watu wote
   B. watoto
   C. watu wazima
   D. vijana

7. Usafi wa mazingira ni kama
   A. kukata kucha
   B. kunawa mikono
   C. kufyeka nyasi
   D. kupiga meno mswaki

8. Chawa huishi katika
   A. nguo safi
   B. nywele chafu
   C. nywele fupi
   D. nguo za ndani

9. Kupenga kamasi ni
   A. kutoa kamasi
   B. kusafisha kamasi
   C. kurundisha kamasi
   D. kupata kamasi

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 10 hadi 12.

Ilikuwa majuto ni mjukuu kwa jamaa mmoja aliyenaswa na wanakijiji kutokana na mazoea yake ya kuchoma nyumba za watu usiku wa manane kwa sababu zisizojulikana. Jamaa huyo alilishwa kichapo ambacho daima hatawahi kisahau maishani.

Inadokezwa kuwa mzee mmoja ambaye hangevumilia vilio vya wanakijiji alisaka usaidizi wa mganga ndipo akamvamia usiku kwenye boma lake akiwa amechanganyikiwa.

10. Kwa nini jamaa aliyenaswa alikuwa akizichoma nyumba za watu?
   A. hazijulikani
   B. alikuwa na wivu
   C. jambo hilo lilimfurahisha
   D. alitumwa na wahalifu

11. Maneno 'alilishwa kichapo' yana maana ya
   A. kutiwa mbaroni
   B. kupigwa sana
   C. alipewa kichapo ale
   D. alichapwa baada ya kula

12. Mzee aliyemnasa jamaa huyo alitafuta usaidizi kwa
   A. daktari
   B. wanakijiji
   C. Mungu
   D. mganga

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 13 hadi 15.

Mtu yeyote huhitaji kuwa na afya nzuri. Wakati mwili unapouma, mtu hawezi kufanya kazi vizuri. Yeye hukosa nguvu na kuwa mnyonge sana.

Je, ni mambo yapi mtu anastahili kufanya ili kuwa na afya nzuri? Kuna mambo mengi ambayo unastahili kuzingatia ili tuwe na afya njema. Jambo la kwanza ni vyakula tunavyokula. Mtu yeyote anafaa kula vyakula bora na safi. Vyakula bora huupa mwili nguvu, vingine hujenga mwili na vipo vya kulinda mwili hasa mboga na matunda.

13. Ni nani anafaa kuwa na afya nzuri?
   A. wadudu
   B. muyonge
   C. kila mtu
   D. mbu

14. Mtu anapoungua
   A. hula vyakula vingi
   B. hufanya kazi nyingi
   D. huwa na nguvu nyingi

15. Ni jambo lipi halisaidii mtu kuwa na afya n
   A. vyakula bora
   B. Usafi wa nyumba
   C. usafi wa mwili
   D. kunguni na chawa

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 hadi 20. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Fisi ni mnyama o ___ 16 ___ sana. Urafiki ___ 17 ___ na sungura ___ 18 ___ alipoanza kula mifugo waliofuga ___ 19___. Akawa akimdanganya sungura ___ 20 ___ mifugo wameliwa na simba.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 16. | A. mpole | B. mkali | C. mjanja | D. mlafi |
| 17. | A. lake | B. yake | C. lao | D. wao |
| 18. | A. ulivunjika | B. umevunjika | C. utavunjika | D. unavunjika |
| 19. | A. kimoja | B. pamoja | C. moja | D. mamoja |
| 20. | A. kua | B. kuwa | C. heti | D. ala |

**Kutoka swali la 21 hadi 30, chagua jibu sahihi**

21. Tumia kivumishi sahihi.
    *Nilianguka ______ sikuumia*
    A. wala
    B. bila
    C. lakini
    D. na
22. Andika umoja wa sentensi ifuatayo
    *Funguo hizi ni zetu.*
    A. Funguo hii ni yetu.
    B. Funguo hii ni yangu.
    C. Ufunguo huu ni wangu.
    D. Ufunguo huu ni wetu.
23. Ni sentensi gani imetumia -enyewe- kwa usahihi.
    A. Gari yenyewe inapendeza
    B. Chai chenyewe ni kitamu
    C. Mtoto mwenyewe ni mwerevu
    D. Kipepeo chenyewe maridadi
24. Nomino 'mti' liko katika ngeli gani?
    A. U - ZI
    B. U - I
    C. I - I
    D. I - ZI
25. Ni sentensi gani iliyoakifishwa vizuri
    A. mji mkuu wa kenya ni nairobi
    B. Mji Mkuu wa kenya ni nairobi
    C. Mji mkuu wa kenya ni Nairobi
    D. Mji mkuu wa Kenya ni Nairobi.
26. Tumia kirejeshi - amba-
    *Kiatu avaacho kinamfaa.*
    A. Kiatu ambacho kinamfaa.
    B. Kiatu ambacho anavaa kinamvaa.
    C. Kiatu ambayo anavaa kinamvaa.
    D. Kiatu ambacho anavaa kinamfaa.
27. Kanusha: Nimemaliza kuandika insha
    A. Hajamaliza kuandika insha.
    B. Nilimaliza kuandika insha
    C. Sijamaliza kuandika insha
    D. Nimemaliza kutoandika insha
28. Chagua sentensi iliyo na kivumishi cha pekee
    A. Watoto wazuri walipewa zawadi.
    B. Magari mengi yatapakwa rangi.
    C. Mwalimu huyu amewasili sasa hivi.
    D. Kitabu chenyewe kimeraruka.
29. Chagua sentensi iliyo katika hali ya mazoea.
    A. wao hupanda miti
    B. gari lilisafiri salama
    C. matunda yataletwa kesho
    D. uvumi umekuwa mwingi.
30. Chagua nomino ya makundi isiyofaa.
    A. Safu ya milima.
    B. Baraza la wazee.
    C. Wingu la moto.
    D. Thurea ya nyota.

**KUANDIKA : INSHA**

**Andika insha juu ya :**

**"SIKU YANGU YA KUZALIWA"**